Current

# KATIBA YA CHAMA CHA UPDP

UPDP

[redacted]

# KATIBA YA UPDP

# YALIYOMO


Utangulizi 1
Tafsili 4
Imani ya chama 4
Madhumuni ya Chama 8

**SEHMEU YA PILI**
Uanachama 11
Kutoka Uanachama 13
Sifa za kuwa kiongozi katika chama 13
Uongozi katika Chama 16
Kukoma Uongozi 16

**SEHEMU YA TATU**
Ngazi za chama 17
Uongozi ngazi ya kitaifa 17

**SEHEMU YA NNE**
Uongozi wa chama ngazi ya Shina 18
Uongozi wa chama ngazi ya Kitongoji 19
Uongozi ngazi ya tawi 20
Uchaguzi na wadhifa wa Mweka Hazina wa Tawi 21
Uongozi ngazi ya Kata 21
Uchaguzi wa wadhifa wa Mweka Hazina wa Kata 22
Uongozi ngazi ya Wilaya 23
Uchaguzi na wadhifa wa Mweka Hazina wa Wilaya 24
Uongozi ngazi ya Mkoa 24
Uchaguzi wa wadhifa wa Mweka Hazina wa Mkoa 26
Uongozi wa Taifa 26
Uchaguzi wa wadhifa wa M/kiti - TAIFA 26
Uchaguzi na wadhifa wa makamu M/Kiti Taifa 29
Uchaguzi wa wadhifa wa Katibu Mkuu Taifa 30
Uchaguzi wa wadhifa wa Naibu Katibu Mkuu Taifa 34
Uchaguzi wa wadhifa wa Mweka Hazina Taifa 36
Uchaguzi wa wadhifa wa Naibu Mweka Hazina Taifa 39





**SEHEMU YA TANO**
Vikao vya Chama 40
Ngazi ya Shina 40
Ngazi ya Kitongoji 41
Ngazi ya Tawi / Sheha 41
Ngazi ya Kata 41
Ngazi ya Wilaya 41
Ngazi ya Mkoa 42
Ngazi ya Taifa 42
NGAZI YA SHINA 42
Kazi ya Mkutano Mkuu wa wanachama wote wa shina 43
Wajumbe wa Kamati ya uongozi wa shina 44
Kazi ya kamati ya uongozi wa shina 44
Ngazi ya Kitongoji 45
Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wanachama wote 46
Kazi za Mkutano Mkuu wa Wanachama wote ktk Kitongoji 46
Wajumbe wa Kamati ya uongozi 48
Kazi za kamati ya Kitongoji 48
NGAZI YA TAWI 49
Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Tawi 50
Kazi za Mkutano Mkuu wa Tawi 50
Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Tawi 52
Kazi za Halmashauri Kuu ya Tawi 52
Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Tawi 54
Kazi za kamati ya utendaji ya Tawi 54
NGAZI YA KATA 56
Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata 56
Kazi za mkutano Mkuu wa Kata 57
Wajumbe wa halmashauri ya Kata 58
Kazi za halmashauri Kuu ya Kata 58
Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kata 59
Kazi za kamati ya utendaji ya Kata 60
NGAZI YA WILAYA 61
Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya 61

Kazi ya Mkutano Mkuu wa (W) 62
Wajumbe wa Kamati ya Utendaji (W) 63
Kazi ya Kamati ya Utendaji ya Wilaya 63
NGAZI YA MKOA 65
Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa 65
Kazi za Mkutano Mkuu wa Mkoa 66
Wajumbe wa H/Kuu ya Mkoa 67
Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa 68
Kazi za Kamati ya Utendaji ya Mkoa 69
NGAZI YA TAIFA 70
Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa 71
Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa 71
Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa 74
Kazi za Halmashauri Kuu ya Taifa 74
Wajumbe wa Kamati Kuu ya Taifa 79
Kazi za Kamati Kuu ya Taifa 79
Kamati ya utendaji ya Kamati Kuu ya Chama Taifa 82
Wajumbe wa Kamati ya utendaji ya Kamati Kuu ya Taifa 83
Kazi za Kamati ya utendaji ya Kamati Kuu Taifa 83
KURUGEZI ZA IDARA MBALIMBALI 84
Mkutano wa dharura wa Chama (T) 85
Fedha na mapato ya Chama 85
MENGINEYO 86
Kazi za Wadhamini wa Chama 86
Mashirikisho ya Chama 88
Shirikisho la Vijana 89
Shirikisho la Wanawake 89
Shirikisho la Wazazi 90
Haki za Wanachama 91
Wajibu wa Wanachama 92
Kanuni za Chama 93
Kamati ya nidhamu 97
Wajumbe wa Kamati ya nidhamu ya Chama Taifa 98
Kazi za kamati ya nidhamu ya Chama Taifa 98
Utaratibu wa kuchagua wagombea nafasi za uongozi 99
Maadili ya utawala na uongozi 100




# UNITED PEOPLES DEMOCRATIC PARTY (UPDP)

## UTANGULIZI.

Sisi wana UPDP tumeamua kufuata mfumo wa kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kijamii wa Demokrasia ya Kijamaa (socialist democracy). Baada ya kubaini mifumo mingine yote imeshindwa kumjengea mwanadamu amani, utulivu na furaha.

Dunia yetu hii kuna mifumo mitatu maarufu ambayo ndio inayofuatwa na mataifa mbali mbali. Mifumo hiyo wa kwanza ni demokrasia ya kibepari (Capitalist democracy) wa pili ni demokrasia ya mapinduzi ya kijamaa (Communist democracy) na tatu demokrasia ya kijamaa (Socialist democracy)

Hivyo sisi wana UPDP tumebaini mifumo miwili kati ya mitatu haifai kwa kuwa imeshindwa kuwahakikishia amani na utulivu wanadamu. Kwamba mfumo wa mapinduzi ya kijamaa umeshindwa kwa kuwa ni mfumo ambao ulikuwa unakinzana na maumbile ya mwanadamu. Kwa kuwa uendeshaji wake ulikuwa tofauti na maumbile ya mwanadamu. Kwa kuwa uendeshaji ulikuwa tofauti na maumbile ya mwanadamu hivyo ni wazi

ulitarafajiwa kushindwa. Kwa kuwa mwandamu ameumbiwa kumiliki mali yake na ukoministi ulikuwa unapiga vita umiliki binafsi. Hivyo mfumo huo wa kikomunisti ulisimikwa katika misingi ya chuki na dhuluma dhidi ya raia kulikofanywa na serikali. Kwa kupora ardhi, Mashamba, Viwanda Mashule Mahospitali nk.

Pia mfumo wa demokrasia ya ubepari haufai na tumebaini umeshindwa kumjengea amani na maendeleo raia. Kwa kuwa haumsaidii mwanadamu kuishi maisha ya amani na utulivu. Amani pekee iko kwa wale wenye kumiliki ardhi kubwa mitaji na uzalishaji. Pamoja na ukweli kwamba ubepari umefanya mabadiliko makubwa na mengi ya kijamii. Lakini mabadiliko hayo bado hayajakidhi huduma za jamii hasa kwa matabaka ya chini ingawa kumefanyika mabadiliko kwenye kanuni; Hivyo bado ubepari unaendeshwa kwa nguvu za kibeberu duniani. Sera zote za utekelezaji wa demokrasia ya kibepari zinaratibiwa na ubeberu. Ubeberu ndio unaotafuta rasilimali ardhi na soko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa katika Mataifa yao na kuwahakikishia maisha ya amani na utulivu raia zao. Kwa kutumia ubeberu ubepari umefanikiwa kujitwalia vibaraka katika nchi yetu. Na vibaraka hao



utawakuta na kuwashuhudia kwenye uandikaji na utiaji saini mikataba na uuzaji wa ardhi yetu na hatimaye wananchi kuitwa wavamizi ndani ya maeneo yao ya asili na nchi yao.

Sisi UPDP tumeamua kwamba mfumo bora ni demokrasia ya kijamaa. Mfumo wa kidemokrasia kijamaa ndio pekee ambao unaheshimu utu wa mtu, mali ya mtu yoyote ikiwamo ardhi. Mwananchi au raia hataporwa ardhi kwa sababu yoyote isipokuwa kwa ridhaa yake. Mfumo wa demokrasi ya kijamaa ndio pekee utakaotoa nafuu ya kodi kwa tabaka la chini na matajiri kulipa zaidi ili kuchangia huduma za kijamii ambazo ni matibabu, elimu na chakula. Kila raia lazima apate huduma za msingi bila ya pingamizi na kusimamiwa utekelezaji wake. Sisi wana UPDP misingi ya Imani yetu ni kupambana ili kuondoa njia zote za ukandamizaji, dhuluma dhidi ya mtu na mtu mwingine, pia tutapambana ili kuondoa njia zote za dhuluma zinazofanywa na madhalimu na vibaraka wao. Na tunadhamira ya kujenga jamii ya kijamaa ambayo watu wote watatendeana kama ndugu katika Taifa la Tanzania.

Kwa kauli moja wana UPDP tutafuata na kusimamia maadili ya demokrasia ya kijamaa.

## 1.0 TAFASILI:

1.1 Jina la chama kwa kiingereza litakuwa **UNITED PEOPLES DEMOCRATIC PARTY (UPDP)**

1.2 MAKAO MAKUU YA CHAMA yatakuwa ZANZIBAR au upande wowote katika Jamhuri ya Muungano.

1.3 CHAMA KITAKUWA NA BENDERA yake yenye rangi tatu (3) KIJANI ISIYOIVA (LIGHT GREEN) BLUU NA NYEUPE pamoja na alama ya chama katikati.

1.4 CHAMA KITAKUWA NA NEMBO nayo ni HINDI lililosimama, SHADA la karafuu na jina la chama (UPDP)

1.5 CHAMA kitakuwa na miradi yake ya kilimo, viwanda, Biashara n.k

1.6 CHAMA kitakuwa na mashirikisho ya vijana, wanawake na wazazi ambayo yatafanya kazi chini ya chama kwa kila ngazi.

## 2.0 IMANI YA CHAMA:

2.1 Chama kinaamini katika ujenzi wa misingi ya demokrasia ya kijamaa (socialisti democracy)



2.2 Misingi ambayo italindwa na ujenzi wa amani na mageuzi ya kijamii katika kulinda ardhi mali na rasilimali.

2.3 Ili tuendelee tunahitaji mambo manne (4)

(a) Ardhi imilikiwe na wananchi na kuiondoa mikononi mwa serikali

(b) Watu wenye afya na lishe bora

(c) Uongozi usiokuwa na hila

(d) Usimamizi bora katika uzalishaji na huduma

2.4 Ili tuendelee, tunahitaji amani ambayo italeta mageuzi katika jamii.

2.5 Chama cha UPDP, kinaamini kwamba binadamu wote ni sawa kiheshima na kila raia wa Nchi hii anayo haki kushiriki katika ngazi zote za serikali.

2.6 Kila raia wa Nchi hii, anayo haki ya kuamua, kusafiri, kuabudu dini anayotaka na kukutana na mtu yeyote anayetaka kama katika kufanya hivyo

atakuwa hajihusishi na videndo vyenye kuvunja sheria ama kudhoofisha heshima ya chama au ya mtu mwingine.

2.7 Utukufu wa mtu, sura ya mtu, rangi ya mtu au mahali alipozaliwa haitakubalika iwe dira ya kubagua ama kumdhalilisha mtanzania mwingine

2.8 Usalama, umoja, masikilizano, Amani ndani ya Nchi hii ni mambo pekee yatakayoweza kuleta maendeleao ya nchi na wananchi wa Nchi hii.

2.9 Kwamba kila raia anayo haki ya kupata malipo ya haki sawa kwa kazi atakayofanya na kipato ambacho kitakachomsaidia yeye a na familia yake.

(a) Ni kosa kwa watu wanaofanya kazi ya aina moja kuwabagua katika malipo ya mshahara kutegemea rangi zao, dini zao au sehemu wanakotoka au asili ya mtu.

(b) Kazi maana yake ni njia yeyote ambayo inamuingizia kipato ambacho katika uhanyaji wa kazi hiyo havunji sheria ya nchi.

(c) Chama kitawalinda wananchi wake na kuhakikisha kila mtu anapata kazi na kumlinda asikose kazi ya kumpatia riziki yake.

(d) Haki za binadamu ndio zitakuwa msingi wa usimamizi na utoaji wa huduma katika ngazi mbali mbali za chama kama zilivyoainishwa katika tamko la kimataifa la haki za binadamu Duniani.

2.10 Mbali na kueneza sera za chama, ni wajibu wa kila ngazi ya uongozi wa chama kuelimisha jamii juu ya elimu ya uraia ili kuwawezesha wanajamii kuwa na uelewa na ufahamu wa

kutosha kuhusu haki zao za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

## 3.0 MADHUMUNI YA CHAMA.

3.1 Kushirikiana kuondoa kila aina ya dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa na visasi. Kusimamia uhuru wa Taifa hili na raia zake na kuweka heshima ya kila binadamu.

3.2 Kudumisha na kulinda muungano wa Tanzania na kuitetea historia ya nchi yetu na vizazi vyake.

3.3 Kuhakikisha ardhi inamilikiwa na wenyeji hivyo wageni wote wenye nia ya kuwekeza mitaji na uzalishaji katika ardhi watafanya hivyo kwa kushirikiana na wenyeji na serikali itasimamia sheria na kanuni.

(a) Kuona kuwa chama kitasaidia ukuaji wa soko huria na umiliki binafsi wa kila mtu kulingana na uwezo wake bila kuvunja sheria.

(b) Mali ya mtu haitachukuliwa kwa njia ambayo mwenye mali atatendewa dhuluma isipokuwa kama ametenda kosa au atalipwa



kulingana na thamani ya mali halisi.

3.4 Kuhakikisha kwamba chama cha UPDP kinapiga vita aina zote za dhuluma ukandamizaji uonevu vitisho kudharau na upendeleo

3.5 Misingi yote ya elimu kuanzia ngazi ya shule ya misingi mpaka elimu ya juu itazingatia maadili ya taifa na ustawi wa makabila yaliyopo ili kulinda ustawi wa nchi

3.6 Kiswahili ndio lugha pekee kwa mawasiliano katika ngazi zote za Chama na viongozi wote watatumia lugha ya Kiswahili katika Shughuli zao zote nje na ndani ya nchi

3.7 Kuhakikisha kuwa UPDP inadumisha usalama, umoja maendeleo na amani ya kweli ya Taifa hili . kadhalika wanachama wa UPDP itabidi wakubali hivyo katika kujiunga na chama .

3.8 Kushirikiana kwa dhati na kwa moyo safi na vyama vya siasa katika Tanzania, Bara zima la Afrika kama SERA za vyama hivyo zinahubiri maendeleo ya kweli ya Taifa na bara hili la Afrika, pia kuhakikisha kwamba chama kitakuwa na uhusiano na serikali zingine duniani.

3.9 Kushiriki katika maendeleo ya Taifa na kuinua hali ya uchumi ,kuhakikisha kuwa chama kinatumia vizuri na ipasavyo mali za Taifa hili katika kuwaendeleza raia zake na kuwaondolea dhiki,umaskini,unyonge, maradhi na ujinga.

3.10 Kuhakikisha kuwa Taifa au nchi inajitawala ikiwa na viongozi waliochaguliwa/kuteuliwa na wananchi katika misingi ya demokrasia ya kweli na kutoa nafasi sawa bila ya kujali hali, dini,utaifa au jinsia ya mtu.



3.11 Kuhakikisha uchumi wa Taifa unakuwa mikononi mwa wananchi na wanashirikishwa katika sekta kupitia maeneo mbali mbali ya uchumi ili kuleta uwiano wa Taifa.

3.12 Kuhakikisha kwamba chama kinapigania na kuendeleza demokrasia ya kijamaa na umoja kwa madhumuni ya kuchukua madaraka ya kuongoza nchi.

## SEHEMU YA PILI
## UANACHAMA

**4.0 UANACHAMA:**

4.1 Raia yoyote wa Tanzania mwenye umri unaoanzia miaka kumi na nane (18) na kuendelea anaweza kuwa mwanachama wa UPDP ikiwa atakubali madhumuni na imani ya chama. Chini ya umri uliotajwa ndani ya katiba hii, anaweza kujiunga na shirikisho la vijana wa chama.

4.2 Mwanachama anaweza kujiuzulu uanachama wa UPDP au kusimamishwa ama kufukuzwa wakati

mwanachama huyo awe ametimiza miaka miwili (2) tangu alipoingia kaitka chama. Isipokuwa pale katiba hii itakapo tamkwa vinginevyo.

b) Awe ameonyesha uwezo katika ufunguaji wa matawi / mashina katika eneo husika pia mbunifu, uwajibikaji na uadilifu katika chama.

c) Bila ya kuathiri kifungu cha kwanza cha Ibara hii, sifa ya mwanachama yoyote ya kuomba nafasi ya uongozi ngazi ya Taifa katika chama, lazima awe kada wa chama na awe amekitumikia chama kwa kipindi cha miaka mitano (5) Isipokuwa halmashauri kuu kama itaamua vinginevyo.

d) Adhihirishe mapenzi yake na imani yake kwa chama na wanachma kwa juhudi na vitendo vyake vya kuendeleza na kukuza chama na wanachama wake na awe mtu aliyetosheka na asiwe mtu aliyetawaliwa na tamaa.



e) Awe ni mwanachama asiyeyumba na anaetimiza na kutetea maadili, kanuni na katiba ya chama.

f) Awe tayari kukosolewa pale anapoonyesha mapungufu na awe tayari kujirekebisha.

g) Awe ni mwanachama hai wa chama cha UPDP, na awe ameonyesha uwezo wa nafasi ya kufanya kazi katika kushirikiana kwa kipindi cha uanachama wake.

h) Ni mwiko kwa kiongozi kupinga maamuzi ya chama mahakamani au nje ya vikao vya chama. Maamuzi yoyote yaliyofanywa na vikao halali vya chama na mashirikisho yake haviruhusiwi kuhojiwa nje ya vikao.

i) Awe na njia halali za mapato yake ya kujitosheleza, kwani uongozi wa chama ni wa msingi wa kujitolea.

j) Adhihirishe kuwa ana nidhamu na utii kwa kutekeleza maagizo au maelekezo ya vikao vya chama na viongozi wa chama.

k) Awe na uwezo wa kutunza siri za vikao vya chama.

### 5.3 UONGOZI KATIKA CHAMA.

a) Kila mwanachama anaweza kuwa kiongozi endapo atachaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa katiba hii.

b) Uongozi sio haki ya msingi kwa mwanachama yoyote yule, bali haki ya ziada iliyopo kwa kukidhi matakwa ya katiba.

### 5.4 KUKOMA UONGOZI

a) Kiongozi anaweza kujiuzulu kwa hiari yake

b) Anaweza kufukuzwa iwapo atakuwa ametiwa hatiani na mahakama yoyote ya Tanzania kwa kosa la jinai linalohusiana na wizi, uharibifu na ufujaji wa mali au ardhi ya Nchi.

c) Kiongozi anaweza kuachishwa uongozi kwa sababu zozote ambazo mamlaka inayohusika itaona zinatosha kuchukua hatua hiyo.

d) Anaweza kufukuzwa iwapo atakiuka katiba ya chama, maadili au nidhamu ya chama.

e) Kiongozi aliyeachishwa uongozi anaweza kupewa dhamana nyingine ndani ya chama ama anaweza kurudishiwa uongozi aliyoachishwa endapo mamlaka inayohusika itaona kuwa sababu zinazomfanya achukuliwe hatua zimekoma.



f) Kiongozi aliyefukuzwa anaweza kurejeshwa na kikao kilichomfukuza au cha juu yake, isipokuwa kama hatarejeshwa anaweza kukata rufaa ndani ya chama.

## SEHEMU YA TATU YA KATIBA.

### 6.0 NGAZI ZA CHAMA.

Chama kitakuwa na ngazi kama ifuatavyo:-

6.1 a) Ngazi ya shina
b) Ngazi ya kitongoji
c) Ngazi ya tawi au kijiji
d) Ngazi ya kata
e) Ngazi ya wilaya
f) Ngazi ya mkoa
g) Ngazi ya Taifa.

### 6.2 UONGOZI NGAZI YA KITAIFA.

a) Mwenyekiti wa Taifa

b) Makamu mwenyekti wa Taifa
c) Katibu mkuu Taifa
d) Naibu katibu mkuu Taifa
e) Mweka hazina Taifa
f) Naibu mweka hazina Taifa.

## SEHEMU YA NNE YA KATIBA.

## 7.0 UONGOZI WA CHAMA NGAZI YA SHINA.

### 7.1 UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWENYEKITI (BALOZI) WA SHINA.

**a)** Shina litakuwa na wanachama wasiopungua watano wanaoishi kwenye eneo la nyumba kumi (10)

**b)** Mwenyekiti atakayeitwa Balozi wa shina na katibu wa shina, mweka hazina wa shina, pamoja na wajumbe watatu (3) wa kamati ya uongozi wa shina watachaguliwa na mkutano mkuu wa shina kwa kipindi cha miaka mitano (5) na wanaweza kugombea tena nyadhifa zao kwa kipindi kingine.



**c)** Mwenyekiti (balozi) atakuwa balozi wa vikao vya chama ngazi ya shina. Katibu ataitisha vikao vya chama ngazi ya shina kwa kushirikiana na balozi wa shina. Mkutano mkuu wa shina utakuwa na uwezo wa kumwondoa kiongozi yoyote iwapo utaona kuna haja ya kufanya hivyo.

### 7.2 UONGOZI WA CHAMA NGAZI YA KITONGOJI.

### UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWENYEKITI WA KITONGOJI.

a) Mwenyekiti, Katibu, Mweka hazina, na wajumbe watatu (3) wa kamati ya uongozi wa kitongoji, watachaguliwa na mkutano mkuu wa kitongoji.

b) Mwenyekiti atakuwa mwenyekiti wa vikao vya chama ngazi ya kitongoji, katibu wa kitongoji ataitisha vikao vya chama ngazi ya kitongoji kwa kushirikiana na mwenyekiti wa kitongoji.

c) Mkutano mkuu wa kitongoji utakuwa na uwezo wa kumwondoa kiongozi yeyote iwapo utaona kuna haja ya kufanya hivyo.

7.3 **UONGOZI NGAZI YA TAWI. UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWENYEKITI NA KATIBU WA TAWI.**

a) Mwenyekiti wa tawi atachaguliwa na mkutano mkuu wa tawi, kipindi cha miaka mitano (5) na anaweza kugombea tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

b) Katibu wa tawi atateuliwa na kikao cha kamati ya utendaji ya kata kwa mapendekezo ya halmashauri kuu ya tawi.

c) Mwenyekiti atakuwa mwenyekiti wa vikao vya chama ngazi ya tawi. Katibu ataitisha vikao vya chama ngazi ya tawi kwa kushirikiana na mwenyekiti wa tawi.

d) Mkutano mkuu wa tawi utakuwa na uwezo wa kumwondoa



kiongozi yeyote iwapo utaona kuna haja ya kufnya hivyo.

7.4 **UCHAGUZI NA WADHIFA WA NWEKA HAZINA WA TAWI.**

a) Mweka hazina wa tawi atachaguliwa na kikao cha halmashauri kuu ya tawi. Atakuwa meka hazina wa tawi kwa kipindi cha miaka mitano (5) Na anaweza kugombea tena wadhifa wake kwa kipindi kingine

b) Halmashauri kuu ya tawi itakuwa na uwezo wa kumwondoa ama kumsimamisha kiongozi yeyote iwapo itaona kuna haja ya kufaya hivyo.

7.5 **UONGOZI NGAZI YA KATA. UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWENYEKITI NA KATIBU WA KATA.**

a) Mwenyekiti wa kata atachahuliwa na mkutano mkuu wa kata kwa kipindi cha miaka mitano (5) na anaweza

kugombea taena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

b) Katibu kata atateuliwa na kamati ya utendaji ya wilaya kwa mapendekezo ya halmashauri kuu ya kata. Na anaweza kuteuliwa tene kwa kipindi kingine.

c) Mwenyekiti wa kata atakuwa mwenyekiti ;wa vikao vya chama ngazi ya kata. Katibu kata ataitisha vikao vya chama ngaiz ya kata kwa kushirikiana na mwenyekiti wa kata.

d) Mkutano mkuu wa kata utakuwa na uwezo wa kumwondoa kiongozi yeyote iwapo utaona kuna haja ya kufanya hivyo.

## 7.6 UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWEKA HAZINA WA KATA:

a) Mweka hazina wa kata atachaguliwa na halmashauri kuu ya kata. Atakuwa mweka hazina wa kata kwa kipindi cha miaka mitano (5). Na anaweza



kugombea tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

## 7.7 UONGOZI NGAZI YA WILAYA. UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWENYEKITI NA KATIBU WA WILAYA.

a) Mwenyekiti wa Wilaya, ataachaguliwa na mkutano mkuu wa wilaya kwa kipindi cha miaka mitano (5) Na anaweza kugombea tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

b) Katibu wa Wilaya atateuliwa na kamati ya utendaji ya mkoa kwa mapendekezo ya kamati ya utendaji ya wilaya. Na anaweza kuteuliwa tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

c) Mwenyekiti wa wilaya atakuwa mwenyekiti wa vikao vya chama vya wilaya. Katibu wa wilaya ataitisha vikao vya chama kwa kushirikiana na mwenyekiti wa wilaya.

d) Mkutano mkuu wa wilaya utakuwa na uwezo wa kumwondoa kiongozi iwapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo.

## 7.8 UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWEKA HAZINA WA WILAYA.

a) Mweka hazina wa wilaya atachaguliwa na kamati ya utendaji ya wilaya. Atakuwa mweka hazina wa wilaya kwa kipindi cha miaka mitano (5). Na anaweza kugombea tena wadhifa wake kwa kipindi kingine

b) Kamati ya utendaji ya wilaya itakuwa na uwezo wa kumwondoa ama kumsimamisha kiongozi iwapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo.

## 7.9 UONGOZI NGAZI YA MKOA. UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWENYEKITI NA KATIBU WA MKOA.



a) Mwenyekiti wa mkoa atachaguliwa na mkutano mkuu wa mkoa kwa kipindi cha miaka mitano (5) na anaweza kugombea tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

b) Katibu wa mkoa atachaguliwa na kamati kuu ya Taifa kwa mapendekezo ya halmashauri kuu ya mkoa kwa kipindi cha miaka mitano (5) na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine.

c) Mwenyekiti wa mkoa atakuwa mwenyekiti wa vikao vya chama vya mkoa. Katibu ataitisha vikao vya chama vya mkoa kwa kushirikiana na mwenyekiti wa mkoa.

d) Mkutano mkuu wa mkoa utakuwa na uwezo wa kumwondoa kiongozi iwapo utaona kuna haja ya kufanya hivyo.

### 7.10 UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWEKA HAZINA WA MKOA.

a) Mweka hazina wa mkoa atachaguliwa na halmashauri kuu ya mkoa atashika wadhifa wake kwa kipindi cha miaka mitano (5) anaweza kugombea tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

b) Halmashauri kuu ya mkoa itakuwa na uwezo wa kumwondoa ama kumsimamisha kiongozi iwepo itaona kuna haja ya kufanya hivyo.

### 7.11 UONGOZI WA TAIFA.

a) Mwenyekiti
b) Makamu Mwenyekiti
c) Katibu Mkuu
d) Naibu katibu mkuu
e) Mweka hazina
f) Naibu mweka hazina.

### 7.12 UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWENYEKITI - TAIFA.

a) Mwenyekiti wa taifa, atachaguliwa na mkutano muu wa chama taifa.



b) Atakuwa mwenyekiti wa chama Taifa kwa kipindi cha miaka mitano (5) na anaweza kugombea tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

c) Atakuwa mwenyekiti wa mkutano mkuu wa taifa, halmashauri kuu ya taifa, kamati kuu ya taifa na mkutano wa wadhamini wa chama. Pia atakuwa na uwezo wa kuitisha vikao vya juu vya chama kwa dharura (Mkutano mkuu wa taifa, halmashauri kuu ya taifa, kamati kuu ya taifa na mkutano wa wadhamini). Na anaweza kuchukua hatua za makusudi kwa kukinusuru chama.

d) Atashika nafasi ya juu katika chama na atakuwa msemaji mkuu wa chama.

e) Atapendekeza jina la katibu mkuu na kuliwakilisha katika kikao cha halmashauri kuu kwa uthibitisho.

f) Atakuwa hana uwezo wa kumsimamisha au kumwachisha kiongozi / mwanachama yoyote katika chama isipokuwa pale katiba itakavyoelekeza vinginevyo.

g) Muda wa mwenyekiti ni miaka mitano (5)

h) Atakuwa na kura ya uamuzi (VETO) endapo katika kikao anachokiongoza kura za wajumbe zitafungamana.

i) Anaweza kujiuzuru nafasi yake na kuacha wadhifa wake wakati wowote anapohitaji kufanya hivyo.

j) Atakuwa msimamizi mkuu wa mapato na matumizi ya fedha za chama katika Jamhuri ya Muungano wa Taifa. Na ni mtia saini mkuu wa akaunti za chama katika kutoa fedha.

k) Atateua wajumbe sita (6) kuingia katika halmashauri kuu.



## 7.13 UCHAGUZI NA WADHIFA WA MAKAMU MWENYEKITI – TAIFA.

a) Makamu mwenyekiti wa chama taifa atachaguliwa na mkutano mkuu wa chama taifa.

b) Atakuwa makamu mwenyekiti wa chama taifa katika vikao vikuu vya chama taifa. Mkutano mkuu wa chama taifa, halmashauri kuu taifa, kamati kuu ya chama taifa na mkutano mkuu wa wadhamini wa chama.

c) Atakuwa makamu mwenyekiti wa chama kwa kipindi cha miaka mitano (5) na anaweza kugombea tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

d) Atakuwa mwenyekiti wa vikao vya chama taifa pindi mwenyekiti anapokuwa hayupo.

e) Atakuwa msemaji mkuu wa chama anapokosekana mwenyekiti .

f) Kama mwenyekiti ,makamu mwenyekiti hana uwezo wa kumwachisha au kumsimamisha kiongozi / mwanachama yeyote katika chama.

g) Muda wa makamu mwenyekiti ni miaka mitano (5)

h) Atakuwa msimamizi mkuu wa fedha za chama katika jamhuri ya muungano wa Tanzania na atatia saini akaunti za chama katika kutoa fedha iwapo mwenyekiti anapokuwa hayupo.

i) Anaweza kujiuzulu nafasi yake nakuacha wadhifa wake wakati wowote anapohitaji kufanya hivyo .

## 7.14 UCHAGUZI NA WADHIFA WA KATIBU MKUU WA TAIFA

a) Katibu mkuu wa chama taifa atachaguliwa na kikao cha halmashauri kuu ya chama taifa kwa mapendekezo ya mwenyekiti wa chama taifa .



Na atakuwa na majukumu yafuatayo,

b) Atakuwa katibu mkuu wa chama taifa kwa kipindi cha miaka mitano. (5) Anaweza kuchaguliwa tena wadhifa wake kwa kipindi kingine .

c) Ni mtendaji mkuu wa chama katika shughuli zote za chama

d) Ni katibu wa mikutano yote ya chama taifa .(Mkutano mkuu, wa halmashauri kuu, kamati kuu, kamati ya utendaji ngazi ya taifa na mkutano wa wadhamini wa chama.

e) Atakuwa na wajibu wa kuandaa na kuitisha mikutano yote ya vikao vya chama taifa kwa mujibu wa katiba ya chama kwa kushauriana na mwenyekiti wa chama taifa, na atatunza na kuhifadhi mihutasari ya mikutano yote ya chama ngazi ya taifa.

f) Atamshauri mwenyekiti katika kazi za chama. Atatunza nyaraka zote za chama (OFISINI) na kuleta taarifa zake kama atakavyoelekezwa na vikao vya chama ngazi ya taifa.

g) Atakuwa msimamizi mkuu wa shughuli za utendaji wa chama nchi nzima na atakuwa mfuatiliaji wa utekelezaji wa maamuzi ya vikao vya chama.

h) Ataratibu mbinu mbali mbali za kukipatia chama ushindi katika uchaguzi na kukitangaza chama. Mawasiliano ya chama yatatumwa kwa katibu mkuu,

i) Atakuwa hana uwezo wa kumsimamisha au kumwondoa kiongozi ama mwanachama yeyote katika chama.

j) Ataongoza vikao vya wakurugenzi wa chama.

k) Muda wa katibu mkuu ni miaka mitano (5). Anaweza kusimamishwa na halmashauri kuu ya chama taifa kama imeona kuwa anashindwa kufanya kazi yake ipasavyo kwa ajili ya kuugua kipindi kirefu au kushindwa kutekeleza madhumuni, maazimio na siasa ya chama bila ya sababu muhimu au kama atafungwa kifungo cha muda mrefu kwa makosa binafsi nje ya kisiasa.

l) Anaweza kujiuzulu nafasi yake na kuacha wadhifa wake wakati wowote anapohitaji kufanya hivyo.

m) Bila ya kuathiri masharti ya katiba hii, katibu mkuu ataawajibika kwa mwenyekiti wa chama taifa kuhusu utekelezaji wa madaraka yake.

n) Atafanya kazi nyingine zozote atakazopewa na mkutano mkuu taifa, Halmashauri kuu ya taifa, kamati kuu ya taifa na

mwenyekiti wa taifa na makamu mwenyekiti wa taifa.

o) Endapo katibu mkuu atakuwa hayupo kazini au atashindwa kuhudhuria kikao chochote cha kitaifa nafasi yake na naibu katibu mkuu wa chama taifa.

p) Atakuwa mjumbe wa kamati ya ulinzi na usalama ya chama.

q) Ataongoza kurugenzi ya utawala

## 7.15 UCHAGUZI NA WADHIFA WA NAIBU KATIBU MKUU TAIFA.

a) Naibu katibu mkuu atachaguliwa na halmashauri kuu ya chama taifa kwa mapendekezo ya mwenyekiti wa chama taifa.

b) Atakuwa Naibu katibu mkuu wa chama taifa atakuwa mshauri na msaidizi mkuu wa katibu mkuu wa chama taifa atakuwa mshauri na msaidizi mkuu wa katibu mkuu katika shughuli za chama za kila siku.



c) Atakuwa mtendaji mkuu msaidizi wa shughuli za chama za kila siku na atakuwa na madaraka na kazi za chama atakazoagizwa na katibu mkuu.

d) Atakuwa Naibu katibu mkuu katika vikao vya chma. (Mkutano mkuu, Halmashauri kuu, kamati kuu na mkutano wa wadhamini wa chama.)

e) Atakuwa katibu wa vikao vya chama wakati katibu mkuu anapokuwa hayupo kwa sababu zozote zile.

f) Naibu katibu mkuu wa chama taifa anayeishi Tanzania bara au Visiwani, atahesabika kama katibu mkuu mwenye shughuli zote za chama zinazotendeka ndani ya mikoa yake isipokuwa kwenye vikao vyote vinavyohudhuriwa na katibu mkuu wa chama ingawa upeo wa madaraka ya Naibu katibu mkuu wa chama utakuwa kwa Tanzania nzima

kwa wakati wote wa utendaji wa shughuli za chama.

g) Muda wa Naibu katibu mkuu ni miaka mitano (5) anaweza kuteuliwa tena wadhifa wake. Pia anaweza kusimamishwa na halmashauri kuu taifa iwapo itaona kuwa anashindwa kufanya kazi yake ipasavyo kwa ajili ya kuugua kipindi kirefu au kushindwa kutekeleza madhumuni, maazimio na siasa ya chama bila ya sababu muhimu au kama atafungwa kifungo cha muda mrefu kwa makosa binafsi nje ya shughuli za kisiasa ama za chama.

h) Anaweza kujiuzulu nafasi yake na kuacha wadhifa wake wakati wowote anapohitaji kufanya hivyo.

## 7.16 UCHAGUZI NA WADHIFA WA MWEKA HAZINA WA TAIFA.

a) Mweka hazina wa chama taifa, atachaguliwa na kamati kuu ya



taifa kwa mapendekezo ya Sekretarieti (Kamati ya utendaji ya kamati kuu) ya chama taifa.

b) Atakuwa mweka hazina mkuu wa chama taifa kwa kipindi cha miaka mitano (5) na anaweza kuchaguliwa tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

c) Atatafuta mbinu za kukipatia chama mapato.

d) Atakuwa ndiye mkusanyaji na muhifadhi mkuu wa mahesabu ya chama, mipango ya fedha kwa wanachama, wafadhili na kutoka katika taasisi za chama.

e) Atasimamia akaunti zote za chama zitakazo funguliwa na chama

f) Ataandaa na kuhifadhi mahesabu ya chama (ACCOUNTS BOOK) na nyaraka zote zinazohusika na benki akaunti na ni mtia saini

katika akaunti zote za chama katika kuweka na kutoa fedha.

g) Muda wa mweka hazina ni miaka mitano (5) na anaweza kusimamishwa na Sekretariet ya chama taifa ikiona kuwa anashidwa kufanya kazi yake ipasavyo kwa ajili ya kuugua kipindi kirefu au kushindwa kudhibiti fedha, kutekeleza madhumuni na maazimio ya chama au kutohudhuria yeye binafsi kiasi cha mikutano miwili (2) ya vikao vya chama bila sababu muhimu au kama atafungwa kifungo cha muda mrefu kwa makosa binafsi nje ya shughuli za chama ama za kisiasa.

h) Anaweza kujiuzulu nafasi yake na kuacha wadhifa wake wakati wowote anapohitaji kufanya hivyo.



### 7.17 UCHAGUZI NA WADHIFA WA NAIBU MWEKA HAZINA WA TAIFA.

a) Naibu mweka hazina atachaguliwa na kamati kuu ya taifa kwa mapendekezo ya Sekretarieti ya taifa.

b) Atakuwa naibu mweka hazina wa chama taifa kwa kipindi cha miaka mitano (5) na anaweza kuchaguliwa tena wadhifa wake kwa kipindi kingine.

c) Atafanya kazi za kila siku na atakuwa na madaraka na kazi za chama atakazo agizwa na mweka hazina.

d) Atasimamia akaunti za chama zitakazo funguliwa na chama, pia ataandaa na kuhifadhi mahesabu ya chama (ACCOUNTS BOOK & DOCUMENT) zote zinazohusika na benki akaunti wkaati mweka hazina anapokuwa hayupo.

e) Muda wa Naibu mweka hazina ni miaka mitano (5) anaweza

kusimamishwa na Sekretarieti ya taifa ikiona anashindwa kudhibiti fedha, kutekeleza madhumuni na maadhimio ya chama au kutohudhuria yeye binafsi kiasi cha mikutano muhimu miwili (2) ya vikao vya chama bila sababu muhimu au kamati atafungwa kufungo cha muda mrefu kwa makosa binafsi nje ya shughuli za kisiasa ama za chama.

f) Anaweza kujiuzulu nafasi yake na kuacha wadhifa wake wakati wowote anapohitaji kufanya hivyo.

## SEHEMU YA TANO YA KATIBA

## VIKAO VYA CHAMA.

**8.0 VIKAO VYA UPDP**

Vikao vya UPDP vitakuwa katika ngazi zote za chama na mashirikisho yake kama ifuatavyo:-

**8.1 NGAZI YA SHINA.**

Shina litakuwa eneo lote lenye nyumba kumi (10) za kuishi au vituo ishirini vya biashara.



**8.2 NGAZI YA KITONGOJI**

Katika maeneo ya kijiji, kutakuwa na ngazi ya kitongoji ambayo itajumuisha eneo lote la kitongoji lililo chini ya mwenyekiti mmoja wa serikali ya kitongoji.

**8.3 NGAZI YA TAWI/SHEHA**

a) Katika maeneo ya vijiji vya Tanzania bara, tawi litakuwa eneo lote la kijiji lililo chini ya mwenyekiti wa serikali ya kijiji.

b) Katika maeneo ya mijini ya Tanzania Bara, tawi litakuwa ni eneo lote la mtaa lililo chini ya mwenyekiti wa serikali ya mtaa.

c) Kwa Tanzania visiwani, tawi litakuwa ni eneo lote la sheha lililo chini ya uongozi wa serikali ya sheha.

**8.4 NGAZI YA KATA.**

Eneo lote la kata lililo na diwani.

**8.5 NGAZI YA WILAYA.**

Wilaya itakuwa ni eneo lote lililo chini ya Mkuu wa Wilaya wa Serikali.

8.6 **NGAZI YA MKOA.**

Ngazi ya mkoa itajumuisha eneo lote la mkoa lililo chini ya Mkuu wa Mkoa wa serikali.

8.7 **NGAZI YA TAIFA.**

Ngazi ya Taifa itakuwa ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 9.0 NGAZI YA SHINA.

9.1 Shina litakuwa na wanachama wasiopungua watano (5) wanaoishi kwenye eneo lenye nyumba kumu (10) au wanachama watano (5) wanaofanya biashara kwenye eneo lenye vituo vya biashara.

9.2 Katika shina kutakuwa na vikao vifuataavyo:-

a) Mkutano mkuu wa wanachama wote

b) Kamati ya uongozi

c) Kamati ya ulinzi na usalama.

d) Mashirikisho ya chama
   - i) Shirikisho la vijana
   - ii) Shirikisho la wanawake
   - iii) Shirikisho la wazazi



9.3 Wajumbe wa mkutano mkuu wa wanachama wote.

a) Balozi wa shina

b) Katibu wa shina

c) Wanachama wote katika shina

9.4 **KAZI ZA MKUTANO MKUU WA WANACHAMA WOTE WA SHINA.**

a) Kumchagua mwenyekiti atakayeitwa balozi wa shina.

b) Kumchagua katibu wa shina

c) Kuchagua wajumbe wawili (2) wa kamati ya uongozi wa shina.

d) Kuchagua wenyeviti na makatibu wa mashirikisho ya chama (vijana, wanawake na wazee)

e) Kuchagua wajumbe watatu(3) wa kamati ya ulinzi na usalama.

f) Wakati wa uchaguzi, kuhakikisha kwamba wananchi wote katika eneo lao wamejiandikisha kupig akura na wanajitokeza kupiga kura.

g) Kueneza sera za UPDP kaitka ngazi ya shina na nje ya shina.

h) Kushawishi wananchi waliofikia umri wa miaka kumi na nane (18) kujiunga UPDP.

i) Mkutano mkuu wa wanachama wote wa shina utafanyika mara moja kila baada ya miaka mitano (5) au wakati wowote ikiwa ni lazima.

**9.5 WAJUMBE WA KAMATI YA UONGOZI WA SHINA.**

a) Balozi wa shina
b) Katibu wa shina
c) Mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama
d) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama katika shina
e) Wajumbe wawili (2) wa kamatsi ya uongozi **waliochaguliwa na mkutano mkuu wa wanachama wote.**

**9.6 KAZI ZA KAMATI YA UONGOZI YA SHINA.**

a) Kuandaa orodha ya wanachama kila mara katika shina



b) Kuandaa orodha ya wapiga kura wote katika shina na kushawishi wajiandikishe na wapige kura.
c) Kubuni mbinu za kuwaelimisha wananchi wote katika shina lao juu ya sera, itikadi na katiba ya chama
d) Kusimamia shughuli zote za kila siku za chama katika shina
e) Kamati ya uongozi ya shina itakutana mara moja kila mwezi au wakati wowote ikiwa ni lazima.
f) Kuhakikisha kwamba mashirikisho ya chama katika shina yanafanya vikao vyao kwa mujibu wa kanuni zao.
g) Kuratibu na kusimamia shughuli za mashirikisho ya chama katika shina.

**10.0 NGAZI YA KITONGOJI.**

10.1 Katika kitongoji kutakuwa na vikao vifuatavyo:-

a) Mkutano mkuu wa wanachama wote.
b) Kamati ya uongozi

moja kila baada ya miezi sita (6) au wakati wowote ikiwa ni lazima.

### 10.4 WAJUMBE WA KAMATI YA UONGOZI.

a) Mwenyekiti wa kitongoji
b) Katibu wa kitongoji
c) Mweka hazina wa kitongoji
d) Mwenyekiti wa serikali ya kitongoji aliyechaguliwa kwa tiketi ya UPDP.
e) Wajumbe watatu (3) waliochaguliwa na mkutano wa wanachama wote.
f) Wenyeviti na makatibu wa mashirikisho ya chama (vijana, wnawake na wazazi).
g) Mwenyekiti na katibu wa kamati ya ulinzi na usalama katika kitongoji.

### 10.5 KAZI ZA KAMATI YA KITONGOJI

a) Kushawishi wananchi wenye uwezo wa kugombea uongozi wa kigongoji kwa tiketi ya UPDP



b) Kuweka orodha ya wanachama wote wa UPDP katika kitongoji.
c) Kuwa na orodha ya wananchi wote wanaoishi katika kitongoji wenye haki ya kupiga kura.
d) Kuwashawishi wananchi kujiunga na UPDP na kusimamia ufungaji wa mashina ya chama.
e) Kuhakikisha mwamba mashirikisho ya chama katika kitongoji zinafanya vikao vyao kwa mujibu wa kanuni zao.
f) Kamati ya uongozi wa kitongoji itakutana mara moja (1) kila mwezi au wakati wowote ikiwa ni lazima.

## 11.0 NGAZI YA TAWI.

### 11.1 TAWI LITAKUWA NA VIKAO VIFUATAVYO:-

a) Mkutano mkuu wa tawi
b) Halmashauri kuu ya tawi
c) Kamati ya utendani ya tawi
d) Mashirikisho ya chama (vijana, wanawake na wazazi)

## 11.4 WAJUMBE WA HALMASHAURI KUU YA TAWI.

a) Mwenyekiti wa tawi
b) Katibu wa tawi.
c) Mweka hazina wa tawi
d) Wajumbe watatu (3) wa halmashauri kuu ya tawi waliochaguliwa na mkutano mkuu wa tawi.
e) Wajumbe wawili (2) wa kamati ya utendaji waliochaguliwa na halmashauri kuu ya tawi.
f) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama (vijana, wanawake, wazazi ngazi ya tawi).

## 11.5 KAZI ZA HALMASHAURI KUU YA TAWI.

a) Kuchagua wajumbe wawili (2) wa kamati ya utendaji ya tawi.
b) Kupokea, kusimamia na kubuni mikakati mbali mbali ya kutekeleza taarifa za chama katika tawi.
c) Kusimamia uundwaji uongozi wa mashina na vitongoji katika tawi.



d) Kuhimiza wananchi kujiandikisha na kupiga kura wakati wa uchaguzi.
e) Kusikiliza malalamiko juu ya uongozi wa mashina na vitongoji na kuchukua hatua za kinidhamu pale itakapobidi. Anaechukuliwa hatua anaweza kukata rufaa kwenye kata.
f) Kutetea sera na itikadi ya chama kabla na baada ya wakati wa kampeni za uchaguzi.
g) Kuhimiza na kusimamia ahadi zilizotolewa na wagombea katika nafasi mbali mbali za uongozi na kufuatilia utekelezaji wake.
h) Kuchagua mweka hazina wa tawi.
i) Kutetea kwa nguvu zote haki za binadamu na haki za wanawake, watoto, wazee na walemavu.
j) Kusimamia matumizi ya fedha katika tawi.
k) Kupitia majina ya wagomhea serikali za vitongoji na kutoa mapendekezo kwa mkutano mkuu wa tawi kwa uteuzi wa mwisho.

l) Halmashauri kuu ya tawi itakutana mara moja (1) kila baada ya miezi mitatu (3) au wakati wowote ikiwa ni lazima.

m) Halmashauri kuu tawi itakuwa na uwezo wa kusimamisha kiongozi yeyote iwapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo.

## 11.6 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI YA TAWI.

a) Mwenyekiti wa tawi
b) Katibu wa tawi
c) Mweka hazina wa tawi
d) Wajumbe wawili (2) waliochaguliwa na halmashauri kuu ya tawi.
e) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama (vijana, wanawake, wazazi ya tawi)

## 11.7 KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI YA TAWI

a) Kusimamia utekelezaji wa kazi za kila siku za chama katika tawi



b) Kutoa mapendekezo ya uteuzi wa katibu wa tawi kwenye kamati ya utendaji ya kata.

c) Kufanya kampeni wakati wa kipindi cha uchaguzi na kuhakikisha kwamba chama kinapata ushindi.

d) Kuongoza harakati za kupinga uonevu unaoweza kufanywa na serikali kwenye ngazi ya tawi.

e) Itaanzisha na kuratibu miradi ya maendeleo na mapato ya tawi. Pia itakuwa na uwezo wa kufungua akaunti za chama ngazi ya tawi.

f) Itakuwa na uwezo wa kumsimamisha kiongozi yeyote iwapo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo.

g) Itaweka mikakati ya kuongeza idadi ya wanachama wa tawi kama itakavyokuwa imeamualiwa na halmashauri kuu ya tawi au mkutano mkuu wa tawi.

h) Kamati ya utendaji itakutana mara moja (1) kwa kila mwezi au wakati wowote ikiwa ni lazima.

## 12.0 NGAZI YA KATA.

### 12.1 KATA ITAKUWA NA VIKAO VIFUATAVYO;-

a) Mkutano mkuu wa kata
b) Halmashauri kuu ya kata
c) Kamati ya utendaji ya kata
d) Mashirikisho ya chama ngazi ya kata.

### 12.2 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA KATA.

a) mwenyekiti wa kata
b) Katibu wa kata
c) Mweka hazina wa kata
d) Wenyeviti na makatibu wa chama wa matawi yaliyomo katika kata.
e) Wenyeviti na makatibu wa vitongoji vilivyomo katika kata
f) Wajumbe watatu (3) wa halmashauri kuu ya kata
g) Wajumbe wawili (2) wa kamati ya utendaji ya kata.



h) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama ngazi ya kata (vijana, wanawake na wazazi)

### 12.3 KAZI ZA MKUTANO MKUU WA KATA.

a) Kumchagua mwenyekiti wa kata
b) Kuwachagua wajumbe watatu (3) wa halmashauri kuu ya kata
c) Kutangaza majina ya wagombea uenyekiti wa serikali za vitongozi, vijiji na mitaa.
d) Kupiga kura ya mapendekezo ya uchanguzi wa diwani.
e) Kutoa miongozo na mikakati inayohusu maendeleo ya chama katika kata.
f) Kupima utekelezaji wa shughuli za chama matawini, na kuweka mikakati ya ushindi na kuimarisha chama
g) Mkutano mkuu utakuwa na uwezo wa kumwondoa kiongozi yeyote iwapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo.

h) Mkutano mkuu wa kata utafanyika mara mbili (2) kila baada ya mwaka au wakatia wowote ikiwa ni lazima.

12.4 **WAJUMBE WA HALMASHAURI KUU YA KATA.**

a) Mwenyekiti wa kata
b) Katibu wa kata
c) Mweka hazina wa kata
d) Wajumbe watatu (3) waliochaguliwa na mkutano mkuu wa kata
e) Wajumbe wawili (2) wa kamati ya utendaji ya kata waliochauliwa na halmashauri kuu.
f) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama (vijana, wanawake, wazazi)

12.5 **KAZI ZA HALMASHAURI KUU YA KATA.**

a) Kuchagua wajumbe wawili (2) wa kamati ya utendaji ya kata
b) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za chama katika kata



c) Kusimamia kwa karibu utekelezaji wa sera za chama katika kata.
d) Kuhamasisha wananchi kwenda kujiandikisha na kupiga kura na kugombea uongozi.
e) Kupokea taarifa za uhamasishaji na uimarishaji wa chama katika kata.
f) Halmashauri kuu ya kata itakuwa na uwezo wa kumsimamisha au kumwondoa kiongozi yeyote iwapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo.
g) Halmashauri kuu ya kata itakutana mara moja (1) kila baada ya miezi miwili (2) au wakati wowote ikiwa ni lazima.
h) Itachagua mweka hazina wa kata.

12.6 **WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI YA KATA.**

a) Mwenyekiti wa kata
b) Katibu wa kata
c) Mweka hazina wa kata
d) Wajumbe wawili (2) waliochaguliwa na Halmashauri

Kuu ya kata wa kamati ya utendaji kata.

e) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama (vijana, wanawake, wazazi) ngazi ya kata.

## 12.7 KAZI ZA KAMATI YA UTENDANI YA KATA.

a) Kutathimini maendeleo ya shughuli za chama katika kata na kuishauri halmashauri kuu ya kata.

b) Kufuatilia ahadi zilizotolewa na wagombea uongozi wa serikali kwa tiketi ya UPDP na kuishauri halmashauri kuu ya kata.

c) Kusimamia shughuli za kila siku za utekelezaji katika chama ndani ya kata.

d) Kubuni mikakati ya kuhamasisha watu kwa shabaha ya kutafuta kuungwa mkono na kushawishi wananchi kugombea nafasi mbali mbali kwa tiketi ya UPDP.

e) Kufuatilia matatizo ya kijamii katika kata kwa madhumuni ya kuandaa sera ya chama, kupendekeza majina ya madiwani wa viti maalum.

f) Kuamua juu ya matatizo na rufaa kutoka ngazi ya chini.

g) Kuteua makatibu wa chama ngazi ya matawi

h) Kutoa mapendekezo ya wagombea udiwani ngazi ya kata.

i) Kamati ya utendaji itakutana mara moja (1) kwa mwezi au wakati wowote ikiwa ni lazima.



# 13.0 NGAZI YA WILAYA.

## 13.1 WILAYA ITAKUWA NA VIKAO VIFUATAVYO

a) Mkutano mkuu wa wilaya

b) Kamati ya utendaji ya wilaya.

c) Mshirikisho ya chama (vijana, wanawake na wazazi)

## 13.2 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA WILAYA.

a) Mwenyekiti wa wilaya

b) Katibu wa wilaya

c) Mweka hazina wa wilaya
d) Wenyeviti wa mshirikisho ya chama ngazi ya wilaya (vijana, wanawake na wazazi)
e) Wajumbe watatu (3) wa kamati ya utendaji ya wilaya.

### 13.3 KAZI ZA MKUTANO MKUU WA WILAYA.

a) Kumchagua mwenyekiti wa wilaya
b) Kuchagua wajumbe watatu (3) wa kamati ya utendaji ya wilaya
c) Kutoa miongozo na mikakati inayohusu chama wilaya.
d) Mkutano mkuu wa wilaya utakuwa na uwezo wa kumwondoa kiongozi yeyote wa ngazi ya wilaya iwapo kutakuwa na sababu za kufanya hivyo.
e) Mkutano mkuu wa wilaya utafanyika mara moja (1) kila mweka au wakati wowote ikiwa ni lazima.
f) Itasimamia na kuratibu shughuli zote za majimbo kwa kuweka



utaratibu unaoona unafaa kwa kurahishisha utendaji wake.

### 13.4 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI WA WILAYA.

a) Mwenyekiti wa wilaya
b) Katibu wa wilaya
c) Mweka haizna wa wilaya
d) Wajumbe wawili (2) waliochaguliwa na mkutano mkuu wa wilaya.
e) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama ngazi ya wilaya (vijana, wanawake, na wazazi).

### 13.5 KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI YA WILAYA.

a) Kutekeleza shughuli za kila siku za chama wilayani.
b) Kupokea taarifa za utendaji wa chama ngazi za kata.
c) Kuchagua mweka hazina wa wilaya.
d) Kuweka mikakati ya kampeni za uchaguzi katika wilaya

e) Kuratibu shughuli za chama kwenye wilaya.

f) Kuteua wagombea wa uongozi wa chama ngazi ya kata. Kamati ya utendaji hailazimiki kutoa sababu kwa mgombea yeyote kwa kutoteuliwa kwake.

g) Kuamua juu ya rufaa zinazotoka ngazi za chini.

h) Kuteua madiwani wa viti maalum kwa mapendekezo ya kamati ya utendaji ya kata.

i) Kuteua na kutangaza majina ya wagombea udiwani baada ya kupata maoni ya kamati za utendaji ngazi ya kata.

j) Kupitia na kutoa maoni juu ya wagombea ubunge/uwakilishi katika majimbo ya wilaya na kuyapeleka ngazi ya mkoa. Pia inawahusu wabunge/ wawakilishi wa viti maalum.

k) Kuteua makatibu wa chama ngazi za kata.

l) Kamati ya utendaji itakuwa na uwezo wa kumwondoa au



kumsimamisha kiongozi yeyote ngazi ya wilaya iwapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo.

m) Kamati ya utendaji ya wilaya itakutana mara moja (1) kila baada ya miezi miwili au wakati wowote ikiwa ni lazima.

## 14.0 NGAZI YA MKOA

### 14.1 MKOA UTAKUWA NA VIKAO VIFUATAVYO:-

a) Mkutano mkuu wa mkoa.
b) Halmashauri kuu ya mkoa
c) Kamati ya utendaji ya mkoa.
d) Mashirikisho ya chama ngazi ya mkoa (vijana, wanawake, wazazi)

### 14.2 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA MKOA.

a) Mwenyekiti wa mkoa
b) Katibu wa mkoa
c) Mweka hazina wa mkoa
d) Wajumbe wawili (2) wa kamati ya utendaji ya mkoa
e) Wajumbe watatu (3) wa halmashauri kuu ya mkoa

f) Wenyeviti, Makatibu ngazi ya wilaya katika mkoa.

g) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama ngazi ya mkoa (vijana, wanawake, wazazi)

## 14.3 KAZI YA MKUTANO MKUU WA MKOA.

a) Kuchagua mwenyekiti wa mkoa

b) Kuchagua wajumbe watatu (3) wa halmashauri kuu ya mkoa.

c) Kupokea taarifa ya maendeleo ya kazi za chama mkoa.

d) Kutoa miongozo na mikakati inayohusu maendeleo ya chama katika mkoa

e) Mkutano mkuu wa mkoa utakuwa na uwezo wa kumwondoa kiongozi yeyote iwapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo.

## 14.4 WAJUMBE WA HALMASHAURI KUU YA MKOA.

a) Mwenyekiti wa mkoa

b) Katibu wa mkoa

c) Mweka hazina wa mkoa



d) Wajumbe watatu (3) waliochaguliwa na mkutano mkuu wa mkoa

e) Wajumbe wawili (2) wa kamati ya utendaji ya mkoa

f) Wenyeviti na makatibu wa chama ngazi ya wilaya zilizopo katika mkoa.

g) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama ngazi ya mkoa (vijana, wanawake, wazazi)

## 14.5 KAZI ZA HALMASHAURI KUU YA MKOA.

a) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na halmashauri kuu ya taifa na mkutano mkuu wa mkoa.

b) Kuteua wajumbe wawili (2) wa kamati ya utendaji mkoa

c) Kutoa mikakati ya utekelezaji wa sera za chama katika mkoa

d) Kuchagua mweka hazina wa mkoa

e) Kuwaandaa wananchi kwa ajili ya chaguzi mbali mbali

kwa lengo la kukiletea chama ushindani.

f) Kupanga matumizi ya chama ya mkoa na kuyasimamia matumizi hayo

g) Kuzisimamia halmashauri kuu za wilaya na kuzifuatilia utendaji wake wa kazi.

h) Halmashauri kuu ya mkoa itakutana mara tatu (3) kwa mwaka.

## 14.6 WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI YA MKOA.

a) Mwenyekiti wa mkoa.
b) Katibu wa mkoa
c) Mweka hazina wa mkoa
d) Wajumbe wawili (2) waliochaguliwa na halmashauri kuu ya mkoa.
e) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama ngazi ya mkoa (vijana, wanawake, wazazi)



## 14.7 KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI YA MKOA.

a) Kuteua makatibu wa chama ngazi ya wilaya
b) Kutekeleza shughuli za kila siku za chama katika mkoa.
c) Kupokea taarifa za utendaji za wilaya na kuzifikisha kwenye halmashauri kuu ya mkoa kwa hatua zaidi.
d) Kusikiliza rufaa mbali mbali na kuzitolea maamuzi kutoka ngazi za wilaya.
e) Kuchuja majina ya wagombea uongozi wa chama (ubunge/ uwakilishi na viti maalum) majimboni kwa nia ya kupata wagombea wenye sifa.
f) Kuteua wagombea uongozi wa chama ngazi ya wilaya.
g) Kuthibitisha na kudhibiti michango yote ya chama mikoani.
h) Kusimamia shughuli za uenezi, uhamasishaji na kampeni mkoani.

i) Kupitia na kutoa maoni juu ya wagombea ubunge/ uwakilishi pamoja na viti maalum na kuyapeleka kwenye kikao cha kamati kuu ya taifa kwa maamuzi.

j) Kamati ya utendaji ya mkoa itakuwa na uwezo wa kumsimamisha kiongozi yeyote iwapo itaona kama kuna haja ya kufanya hivyo. Pia itakuwa na uwezo wa kufungua akaunti za chama ngazi ya mkoa.

k) Kamati ya utendaji ya mkoa itakutana mara moja (1) kila baada ya miezi miwili au wakati wowote ikibidi.

## 15.0 NGAZI YA TAIFA

### 15.1 KUTAKUWA NA VIKAO VYA TAIFA KAMA IFUATAVYO:-

a) Mkutano mkuu wataifa
b) Halmashauri kuu ya taifa
c) Kamati kuu ya taifa
d) Kamati ya utekelezaji ya kamati kuu



e) Mashirikisho ya chama (vijana, wanawake, wazazi)

### 15.2 WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA TAIFA

a) Mwenyekiti wa taifa
b) Makamu mwenyekiti wa taifa
c) Katibu mkuu wa taifa
d) Naibu katibu mkuu wa taifa
e) Mweka hazina wa taifa
f) Naibu mweka hazina taifa
g) Wajumbe wa halmashauri kuu ya taifa.
h) Wajumbe wa kamati kuu ya taifa
i) Wenyeviti na makatibu wa chama ngazi za mikoa.
j) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama ngazi ya taifa (vijana, wanawake, wazazi)

### 15.3 KAZI ZA MKUTANO MKUU WA TAIFA.

a) Wakati wa uchaguzi, utafanya kazi zifuatazo:-

i) Kuchagua mwenyekiti wa chama taifa, pamoja na makamu mwenyekiti wa taifa.

ii) Kuchagua mwanachama mmoja (1) kugombea nafasi ya Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania na mgombea urais Zanzibara.

iii) Kuchagua wajumbe sita (6) wa halmashauri kuu ya taifa.

b) Kupitisha sera za chama, program zake na kushauri utekelezaji wake.

c) Kupokea na kujadili taarifa zote zilizowasilishwa na halmashauri kuu na kutoa maelekezo ya utekelezaji wake kwa kamati zinazohusika.

d) Kumwondoa madarakani kiongozi yeyote kwa mapendekezo ya halmashauri kuu ya taifa. Hii ikimhusu mwenyekiti na makamu



mwenyekit wa taifa lazima muafaka uwe na theluthi mbili (2) ya wajumbe wote wa kikao hicho ambao wanahaki ya kupiga kura. Kwa viongozi wengine wanaweza kuondolewa kwa zaidi ya nusu ya kura za wajumbe wa kikao chicho.

e) Mkutano mkuu wa taifa unaweza kukasimu kazi na mamlaka yake kwa halmashauri kuu ya taifa.

f) Mkutano mkuu wa taifa, utakuwa na uwezo wa kutunga katiba au kubadili sehemu yoyote ya katiba ya chama kwa uamuzi wa zaidi ya nusu ya kura za wajumbe wenye haki ya kupiga kura.

g) Mkutano mkuu wa kawaida utafanyika kila baada ya miaka mitano (5) Lakini unaweza ukafanyika usio wa kawaida kwa kuitishwa na mwenyekiti. Mkutano mkuu wa kawaida ndiyo utakao kuwa mkutano wa uchaguzi na kipindi cha uongozi ndani ya chama kitakoma wakati wa uchaguzi huo.

## 15.4 WAJUMBE WA HALMASHAURI KUU YA TAIFA.

a) Mwenyekiti wa taifa
b) Makamu mwenyekiti wa taifa.
c) Katibu mkuu taifa.
d) Naibu katibu mkuu taifa
e) Mweka hazina wa taifa
f) Naibu mweka hazina wa taifa
g) Wajumbe waliochaguliwa na mkutano mkuu wa taifa.
h) Wajumbea walioteuliwa na mwenyekiti taifa.
i) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama ngazi ya taifa (vijana, wanawake, wazazi)
j) Wajumbe wa kamati kuu ya taifa waliochaguliwa na halmashauri kuu ya taifa.

## 15.5 KAZI ZA HALMASHAURI KUU YA TAIFA.

a) Kutunga sera za maendeleo ya jamii na uchumi zitakazogusa kila sekta na kuziwasilisha kwenye mkutano mkuu wa taifa.



b) Kuteua katibu mkuu wa chama taifa pamoja na naibu katibu mkuu kutokana na mapendekezo ya mwenyekiti wa chama taifa
c) Kuteua mwanachama mmoja (1) kuwa mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania.
d) Kuchagua wajumbe wane (4) wa kamati kuu ya taifa.
e) Wakati wa uchaguzi, halmashauri kuu itafanya kazi zifuatano:
   i) Kupendekeza majina ya wanachama watakaogombea nafasi ya mwenyekiti wa makamu mwenyekiti wa Taifa.
   ii) Kupendekeza majina ya wanachama watakaogombea nafasi za urais wa jamhuri ya muungano wa Zanzibar.
f) Kuandaa ilani ya chama na kutoa msukumo wa kutekeleza

maazimio, maamuzi na ahadi zilizotolewa na viongozi wa ngazi za juu wa chama au vikao vinavyohusika.

g) Kutekeleza sera za chama kama zilivyokubaliwa na mkutano mkuu wa chama taifa.

h) Kuweka ufuatiliaji wa kutosha wa mkoa hadi mkoa kuhakikisha kwamba sera za chama zinatekelezwa kikamilifu na kuzaa mtaunda yaliyokusudiwa.

i) Kutathimini utekelezaji wa shughuli zote za chama nchini.

j) Kujadili makala za kitaalam zilizo andaliwa na kamati kuu ya taifa kuhusu maendelea ya nchi kwa ajili ya kuwasilisha kwenye mkutnao mkuu wa taifa.

k) Kutayarisha kanuni na masharti ya uendeshaji mzuri wa chama.

l) Kuandaa habari zote muhimu kwa ajili ya matumizi ya mkutano mkuu wa taifa.

m) Kuyafikisha maagizo na maazimio ya chama mikoani na



kutoa uamuzi juu ya mapendekezo kutoka vikao vya juu vya chama ngazi za chini yake.

n) Kuziongoza kamati za utendaji za mkioa katika mwenendo bora wa kuimarisha chama na kuratibu shughuli za mikoan kuleta ufanisi.

o) Kuandaa mkutano mkuu wa taifa. Pia kuandaa kanuni na taratibu shughuli za chama kwa ngazi zote.

p) Kushauri ama kuunda kamati au tume kwa shughuli maalumu bila kuathiri majukumu ya kamati kuu ya chama taifa.

q) Kusimamia au kubadili kifungu chochote cha katiba kwa maslahi ya chama. Kuruhusu kifungu kutumika kabla ya kiungizwa ndani ya katiba

r) Kumwondoa madarakani kiongozi yeyote ambaye uchaguzi /uteuzi wake

umefanywa na halmashauri kuu ya taifa.

s) Kupanga makadirio, mapato na matumizi ya chama.

t) Kuandaa na kupitisha kanuni za fedha, uajiri, uchaguzi, nidhamu na utawala.

u) Kupitisha kanuni za mashirikisho ya chama (vijana, wanawake, wazazi)

v) Halmashauri kuu ya taifa, inaweza kukaimu madaraka na kazi yake kwa kamati kuu ya taifa, na itafanya kazi za mkutano mkuu taifa kama itakavyoagizwa na mkutano kuu.

w) Halmashauri kuu ya taifa itakutana mara mbili (2) kwa mwaka katika vikao vya kawaida. Inaweza kukutana wakati wowote kwa dharura endapo itaitishwa na mwenyekiti wa taifa.



## 15.6 WAJUMBEA WA KAMATI KUU YA TAIFA.

a) Mwenyekiti wa taifa
b) Makamu mwenyekit wa taifa
c) Katibu mkuu taifa
d) Naibu katibu mkuu taifa
e) Mweka hazina wa taifa
f) Naibu mweka hazina taifa
g) Wenyeviti wa mashirikisho ya chama ngazi ya taifa (vijana, wanawake, wazazi)
h) Wajumbe wa kamati kuu waliochaguliwa na halmashauri kuu wa taifa.

## 15.7 KAZI ZA KAMATI KUU TAIFA.

a) Kuchagua mweka hazina pamoja na naibu wake kutokana na mapendekezo ya kamati ya utendaji ya kamati kuu ya taifa
b) Kupendekeza mgombea mwenza wa urais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania na kuwasilisha jina kikao cha halmashauri kuu.

c) Kuteua wadhamini wanne (4) wa chama kutokana na mapendekezo ya kamati ya utendaji ya kamati kuu taifa.
d) Kuteua makatibu wa chama ngazi ya mkoa.
e) Kuteua makatibu wa mashirikisho ya chama ngazi ya taifa (vijana, wanawake, wazazi).
f) Kuteua wabunge wa viti maalumu kutokana na mapendekezo ya shirikisho la wanawake taifa.
g) Kutea majina ya wagombea ubunge na uwakilishi
h) Kupendekeza majina ya wagombea uongozi wa chama katika nafasi za juu za kitaifa.
i) Kujaza /kukaimisha nafasi za uongozi zilizowazi kwa kuchagua wanachama wenye sifa (makada) wa kushika nafasi hizo N.B. kwa ngazi za chini za chama, kazi hii itafanywa na kamati za utendaji za chama.



j) Kuandaa mikutano ya halmashauri kuu ya taifa.
k) Kumsimamisha uongozi kiongozi yeyote iliyomteua endapo itathibitika kwamba tabia, utendaji na mwenendo wake vina mwondolea sifa za uongozi.
l) Kutoa uongozi wa siasa, mwelekeo na msimamo wa chama katika nchi.
m) Kulinda haki za wanachama haki za taifa letu kwa kuelekeza nguvu na fikra za viongozi katika kutenda haki zao.
n) Kuchagua marafiki wa chama na wa taifa letu kwa faida ya wote.
o) Kupitisha majina ya wagombea uenyekiti wa mikoa chama na mashirikisho yake.
p) Kupendekeza majina ya wanachma wanaofaa kuwa katibu mkuu wa naibu katibu mkuu kwa mapendekezo ya kamati za utendaji wa kamati kuu ya taifa.

q) Kulinda na kutunza siri za chama pamoja na kuzitetea kwa nguvu zote.

r) Kuandaa mikakati na mbinu za kampeni za uchaguzi na nyinginezo.

s) Kamati kuu ya taifa inaweza kuunda kamati ndogo za chama na kujiwekea utaratibu wake wa kufanya kazi kadri inavyoona inafaa kwa ajili ya kufanikisha shughuli za chama.

t) Itaweza kufanya kazi za halmashauri kuu ya taifa kama itakavyoagizwa.

u) Kamati kuu ya taifa itafanya mikutano yake ya kawaida kila baada ya miezi mitatu (3) isipokuwa inaweza kukutana kwa dharula ikiitishwa na mwenyekiti taifa.

## 16.0 KAMATI YA UTENDAJI YA KAMATI KUU YA CHAMA TIAFA.

16.1. a) Kutakuwa na kamati ya utendaji ya kamati kuu, ambayo itakuwa ndicho chimbuko la uongozi na utawala wa UPDP. Itafanya kazi zote za chama kwa maelekezo na maagizo ya kamati kuu ya chama taifa.

b) Kutakuwa na kamati za utendaji ndogo mbili (2) za kitaifa. Bara na Zanzibar ili kurahisisha utendaji wa shughuli za kila siku za chama kwa kila upande. Na maamuzi yake ni halali.



### 16.2. WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI YA KAMATI KUU TAIFA.

a) Mwenyekiti wa taifa
b) Makamu mwenyekiti taifa
c) Katibu mkuu taifa
d) Naibu katibu mkuu tiafa
e) Mweka hazina taifa
f) Naibu mweka hazina taifa

### 16.3. KAZI ZA KAMATI YA UTENDAJI YA KAMATI KUU TAIFA.

a) Kamati ya utendaji ya kamati kuu, itakuwa na dhamana ya utawala kwa niaba ya kamati kuu ya chama taifa.

b) Itasimamia utekelezaji wa shughuli zote za kila siku za chama. Kujaza

nafasi zilizo wazi katika uongozi kwa kuteua wanachama makada wa kukaimu hadi vikao vinavyohusika na uchaguzi au uteuzi. Kazi hii itafanywa na kamati ndogo za kamati ya utendaji ya kamati kuu taifa za bara na visiwani Zanzibar kulingana na nafasi iliyowazi kwa kila upande. Uteuzi huo utakuwa kwenye kikao cha kamati ya utendaji ya kamati kuu kwa uthibitisho zaidi

c) Itaandaa nakala ya kitaalamu kwa ajili ya kamati kuu.

## 17.0 CHAMA KITAKUWA NA KURUGENZI ZA IDARA MBALI MBALI.

a) Utawala na uendeshaji.
b) Kampeni na uchaguzi
c) Mambo ya nje
d) Uchumi na mipango
e) Ulinzi na usalama.
f) Uenezi, habari na uhamasishaji
g) Mafunzo na taaluma
h) Fedha.
i) Sera, utafiti na nyaraka n.k



## 18.0 MKUTANO WA DHARURA WA CHAMA TAIFA.

18.1 Mwenyekiti wa chama taifa, atakuwa na mamlaka kamili ya kuitisha mkutano ya : Mkutano mkuu taifa, Halmashauri kuu ya tiafa, kamati kuu ya taifa, kamati ya utendaji ya kamati kuu ya taifa na mkutano wa wadhamini wa chama kwa dharura wakati wowote kama ataona kuna haja ya kuitisha kwa manufaa ya chama. Taarifa ya siku ishirini (20) itatolewa kabla ya mkutano. Lakini unaweza kuitishwa wakati wowote na mwenyekiti wa taifa kama kutakuwa na sababu ya kufanya hivyo.

18.2 Kiwango cha mkutano ni idadi ya nusu ya wajumbe pamoja na udhuru.

## 19.0 FEDHA NA MAPATO YA CHAMA.

19.1 Fedha na mapato ya chama yatatokana na:

a) Viingilio, ada za wanachma na ruzuku ya serikali.
b) Michango kutoka kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi

c) Miradi ya uzalishaji mali zitakazo endeshwa na chama.
d) Mikopo kutoka vyombo vya fedha na watu binafsi.
e) Fedha zote za chama isipokuwa kiwango maalumu kilichokubaliwa kwa matumizi ya papo, zitawekwa benki katika akaunti zitakazofunguliwa na chama.

## 20.0 MENGINEYO

### 20.1 WADHAMINI WA CHAMA.

Kutakuwa na wadhamini wa chama wasiopungua wane (4) na wasiozidi wanne (4) kutoka Bara na Visiwani watakaoteuliwa na kamati kuu ya chama taifa kwa mapendekezo ya kamati ya utendaji ya kamati kuu ya taifa.

### 20.2 KAZI ZA WADHAMINI WA CHAMA

a) Wadhamini wa chama watafanya kazi zao chini ya kamati kuu ya taifa na itatoa taarifa zake kwa kikao hicho.



b) Watamiliki, kutunza na kudhibiti mali zote za chama kwa niaba ya wanachama wa UPDP.
c) Mwanachama au kiongozi yeyote anaweza kugombea nafasi udhamini wa chama, na mdhamini wa chama anaweza kugombea tena nafasi hii kipindi kingine.
d) Mdhamini atatumikia wadhifa huo kwa kipindi cha miaka mitano (5) lakini anaweza kuondolewa au kusimamishwa na kamati kuu ya taifa iwapo itaona kuna haja ya kufanya hivyo.
e) Vikao vyote vya wadhamini, isipokuwa vikao vya dharura vitaitishwa na katibu mkuu wa chama taifa, mwenyekiti wa chama taifa atakuwa mwenyekiti wa vikao vyote vya wadhamini.

f) Wadhamini watakutana mara moja (1) kila mwaka . Lakini kikao cha wadhamini kinaweza kuitishwa wakati wowote iwapo kutakuwa na sababu za kufanya hivyo.

## 21.0 MASHIRIKISHO YA CHAMA.

21.1 Kutakuwa na mashirikisho ya chama ambayo yatafanya kazi chini ya chama kwa ngazi zote kama ifauatavyo:-

a) Shirikisho la vijana
b) Shirikisho la wanawake
c) Shirikisho la wazazi

21.2 Mashirikisho ya chama yataundwa katika ngazi zote za uongozi wa chama yaani:-

a) Ngazi ya kitongoji
b) Ngazi ya tawi.shina
c) Ngazi ya kata/wadi
d) Ngazi ya wilaya
e) Ngazi ya mkoa
f) Ngazi ya taifa



### 21.3 SHIRIKISHO LA VIJANA.

a) Kutakuwa na shirikisho la vijana wa UPDP nchi nzima kuanzia kwenye mashina hadi taifa .
b) Umri wa kujiunga ni miaka kumi na nane (18) hadi miaka arobaini (40).
c) Vijana wa UPDP ndio watakuwa chimbuko la kuanzishwa kwa vituo vya uzalishaji wa vijana.
d) Vijana wataunda mfumo wa chipukizi wa UPDP ambao ni vijana wenye umri ulio chini ya miaka kumi na nane (18) nchi nzima.

### 21.4 SHIRIKISHO LA WANAWAKE.

a) Wanawake wote wa UPDP watakuwa wanachama wa shirikisho la wanawake.
b) Shirikiso la wanawake litajiwekea taratibu za kuteua wabunge na madiwani wa viti maalumu na kutangazwa na kamati kuu taifa.

21.5 **SHIRIKISHO LA WAZAZI.**

a) Wanachama waliotimiza umri wa miaka kumi na nane (18) kwa pamoja watаunda shirikisho la wazazi.

b) Shirikisho litakuwa na jukumu la kuona wazazi wanaelezwa jinsi ya kutunza mazingira bora ili wafaidi matunda ya kazi walizozitenda.

21.6 Mashirikisho yote ya chama yataunda kanuni zaidi ambazo hazitapingana na katiba ya chama.

21.7 Kanuni hizo hazitaanza kutumika mpaka zipate kibali cha kamati kuu ya chama taifa.

21.8 Mashirikisho yote katika ngazi zote, zitakuwa zinafanya kazi zao chini ya uongozi wa chama, zitafanya vikao vyao na kutoa taarifa kwa uongozi wa chama katika ngazi inayohusika.

21.9 Ni jukumu la uongozi wa chama katika kila ngazi kuhakikisha kuwa mashirikisho yote yanafanya kazi na vikao kwa mujibu wa kanuni zao.



## 22.0 HAKI ZA WANACHAMA.

22.1 Mwanachama wa chama cha UPDP, atakuwa na fursa sawa na mwanachama yeyote wa kuchaguliwa kushika uongozi katika chama ngazi yoyote.

22.2 Kiongozi anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano (5) baada ya muda wake kumalizika na anaweza kuchaguliwa tena kama anaonekana anakubalika kwa wanachama.

22.3 Mgombea uongozi wowote wa chama sharti awe na umri wa kuanzia miaka ishirini na moja (21) na awe anajua kusoma na kuandika kiswahili.

22.4 Isipokuwa kwa upande ambapo katiba hii imeelekeza vinginevyo, maombi ya uongozi wa serikali kwa tiketi ya chama, atathibitishwa na vikao vya chama.

22.5 Kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli zote za chama zinazomhusu.

22.6 Kuhudhuria katika mjadala wa vikao vya chama na kupiga kura pale anapohusika.

22.7 Kuchagua na kuchaguliwa katika uongozi, ujumbe au uwakilishi wa chama au wa serikali kupitia chama,.

22.8 Kuonana na kiongozi yeyote wa chama kwa kufuata taratibu za chama (itifaki).

22.9 Kujitetea mbele ya chombo chochote cha chama kinachotaka kumchukulia hatua za kinidhamu.

22.10 Kumkosoa kiongozi, mwanachama au mfanyakazi wa chama kwa kufuata taratibu zilizowekwa na chama.

## 23.0 WAJIBU WA MWANACHAMA.

a) Kujua, kukubali, kulinda na kuitetea IMANI NA MADHUMUNI YA CHAMA popote alipo.

b) Kukieneza chama na siasa yake kwa kadri ya uwezo wake wote.

c) Kukiunga mkono chama kwa kuwapigia kura wanachama wanaogombea nafasi mbali mbali katika uchaguzi wa serikali.

d) Kuwa mwaminifu kwa chama, kuwa na ushirikiano na wanachama wenzako.

e) Kulinda na kutetea haki za binadamu na haki za watu popote duniani.



f) Mjumbe wa kikao, ni lazima ahudhurie na pale ambapo hatohudhuria kwa sababu maalumu, itabidi amuarifu katibu wa kikao hicho kwa maandishi.

g) Mjumbe anayekosa kuhudhuria vikao vitatu (3) mfululizo bila sababu inayokubalika na ambayo anatakiwa kikatiba ahudhurie, basi ataacha kuwa mjumbe wa kikao na atakauwa amejiondoa mwenyewe.

h) Mwanachama yeyote atawajibika kuheshimu na kuyakubali maamuzi yote ya vikao vyote vya chama. Kukuza moyo na ushirikiano na kuthamini uamuzi wa pamoja.

## 24.0 KANUNI ZA CHAMA.

24.1 Kamati kuu inaweza kutunga kanuni za chama kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa sera na malengo ya chama kwa kuzingatia misingi ya katiba hii.

24.2 Chama kitawasiliana katika shughuli zake zote za ndani na Nje ya nchi kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

24.3 Ila isipokuwa pale ambapo katiba imeeleza vinginevyo.

24.4 Masharti ya kuchaguliwa kiongozi na kipindi cha uongozi kitakuwa kama ifuatavyo:-

a) Kipindi cha uongozi wa chama kitakuwa ni miaka mitano (5). Isipokuwa kama kiongozi ameshindwa kazi aliyopewa.

b) Iwapo kipindi cha uongozi kimemalizika na kuna sababu za msingi za kitaifa kwamba uchaguzi wa viongozi hao hauwezi kufanyika, basi muda wa uongozi utaendelea kwa kipindi kingine cha miezi isiyozidi kumi na mbili (12) na baada ya hapo ni lazima uchaguzi mpya ufanyike / uitishwe.

c) Mwanachama wa chama hiki, atakuwa na fursa sawa na mwanachama yeyote kuchagua na kuchaguliwa kushika uongozi katika chama ngazi yoyote ile kwa taratibu zilizowekwa na katiba hii.

d) Kikao chochote cha chama na ngazi yoyote ile, kinaweza



kuunda tume ya muda kwa ajili ya kuchunguza jambo au kufanya shughuli yoyote itakayoelezwa kufanya na kikao chenyewe na tume iliyoundwa ni lazima iwe na majukumu yaliyo wazi na kupewa muda wa kukamilisha kazi hiyo.

e) Pale iwapo pana nafasi wazi ya wajumbe katika ngazi yoyote ya chama, ngazi ya kamati kuu au kamati tendaji kujaza nafasi hizo haraka na kwa vyovyote si zaidi ya miezi mitatu (3) kwa kufuata utaratibu uliowekwa na katiba hii.

f) Katika katiba hii, maneno yafuatayo yatakuwa na maana iliyopewa mbele yake ila pale ambapo imeelezwa vinginevyo.

g) Kamati kuu ndio chombo cha juu katika kuteua nafasi za wagombea wa ngazi ya taifa. Na kusikiliza rufaa za ngazi ya chini ya chama.

h) Wakati wa uchaguzi wa ndani ya chama kamati kuu haitalazimika kutoa sababu yoyote ile kwa

mwanachama atakayechujwa kugombea nafasi husika.

- **HALMASHAURI KUU:** Ina maana ya kamati kuu ya uongozi katika ngazi inayohusika.

- **HAKI ZA BINADAMU:** Ni haki ambazo mtu yeyote anakuwa nazo tangu kuzaliwa kwake.

- **KAMATI YA UTENDAJI:** Ni sekretarieti ya chama katika ngazi inayohusika ya chama.

- **KIJANA:** Inajumuisha kijana yoyote ambaye atakubaliana na chama kama itakavyoelezwa katika kanuni za chama.

- **MKUTANO MKUU:** Ina maana ya mamlaka ya juu kabisa ya chama na yenye maamunzi kaitka ngazi inayohusika ya chama.



- **MZAZI;** Ina maana ya mwanachama wa chama aliyefikia umri wa miaka kumi na nane (18) awe mwanamke au mwanaume.

- **VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA:** Inajumuisha mwenyekiti wa taifa, makamu mwenyekiti wa taifa, katibu mkuu, naibu katibu mkuu, mweka hazina na naibu mweka hazina taifa.

Katiba hii ni katiba ya **UNITED PEOPLES DEMOCRATIC PARTY.** Na kwa kiingereza ni **THE CONSTITUTION OF THE UNITED PEOPLES DEMOCRATIC PARTY.** Katiba hii imeanza kutumika tarehe:............2010.

**25.0 KAMATI YA NIDHAMU YA CHAMA.**

25.1 Kutakuwa na kamati ya nidhamu ya chama ambayo itaongozwa na katibu mkuu katika ngazi ya taifa.

25.2 Kamati za nidhamu zitaundwa katika ngazi zote za chama kwa kufuata muundo wa kitaifa.

**25.3 WAJUMBE WA KAMATI YA NIDHAMU YA CHAMA TAIFA.**

a) Katibu mkuu wa chama taifa
b) Naibu katibu mkuu wa chama taifa.
c) Wajumbe watatu (3) wa kuteuliwa na kamati kuu taifa.

**25.4 KAZI ZA KAMATI YA NIDHAMU YA CHAMA TAIFA.**

a) Kuhakikisha nidhamu inakuwepo ndani ya chama.
b) Kusimamia maadili ya viongozi wa kitaifa na mikao, isipokuwa mwenyekiti wa chama taifa na makamu wake. Na kutoa mapendekezo kwa vikao vinavyohusika (KAMATI KUU) kwa hatua ziadi.
c) Kuhakikisha viongozi na wanachama wanaheshimu katiba na inafuatwa ili kujenga nidhamu ya kweli.
d) Kamati ya nidhamu itawajibika kwa mwenyekiti wa chama taifa.
e) Kamati ya nidhamu itakutana mara moja kwa miezi sita (6) au wakati wowote ikiwa ni lazima.

**26.0 UTARATIBU WA KUCHAGUA WAGOMBEA NAFASI ZA UONGOZI.**

26.1 Chini ya katiba hii, chombo chochote cha chama, kinaweza kuamua kwamba ni lazima au inafaa uchaguzi wa wajumbe wa chama kwenye ngazi yoyote iliyoundwa na katiba hii kufanyika kwa siri.

26.2 Uchaguzi katika ngazi yoyote, utafuata kanuni za uchaguzi zializopitishwa na kamati kuu ya chama taifa.

26.3 Iwapo uchaguzi utavurugika kwa namna ambayo hauwezi kufanyika kwa siku hiyo viongozi waliojiuzulu nyadhifa zao watarejea katika madaraka hadi hapo utakapofanyika

uchaguzi mwingine kwa siku na tarehe itakayotangazwa.

## 27.0 MAADILI YA UTAWALA NA UONGOZI.

27.1 Imekubaliwa na kupitishwa na vikao vya chama kwamba wanachama wanaoshika nafasi za uongozi wa kuchaguliwa au kuteuliwa, wajibu wao bila mshahara au malipo maalumu ya kimkataba.

27.2 Viongozi watakaoingia mkataba na UPDP kama waajiriwa, mikataba yao itaheshimiwa kwa kadri ya masharti na kanuni za chama zinavyoelekeza.

27.3 Viongozi na wanachama wote kwa pamoja, wanawajibika kutafuta njia mbali mbali za kukiingizia chama mapato yake ili kujiimarisha na kuweza kulipa gharama za kukiwezesha chama kuwepo.